

# UHURU WA MBEGU KWA WAKULIMA!

**U**huru wa mbegu una maana kwamba wakulima wanaweza kudhibiti na wana mamlaka ya mifumo yao ya mbegu.

Wewe kama mkulima utakuwa na 'uhuru wa mbegu' iwapo utakuwa na haki ya kufanya yafuatayo:

- ◆ kuotesha, kuzalisha, kuhifadhi na kubadilishana aina zote za mbegu na vipandikizi vingine;
- ◆ kushiriki katika maamuzi yanayohusu kuboresha/kuzalisha mbegu, kuchagua, viwango vya ubora, kupanga bei, uzalishaji, usambazaji na anuwai;
- ◆ desturi za kimila hasa kuhusiana na mbegu za asili;
- ◆ upatikanaji wa mbegu;
- ◆ kulindwa usiuziwe mbegu bandia na zisizofaa;
- ◆ kuwa na uamuzi wa kweli baina ya matumizi ya mbegu zilizothibitishwa na mbegu kutoka kwenye mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima; na
- ◆ kutekeleza haki yako ya mkulima ambayo haipaswi kuwa chini kwa hadhi ya ile ya haki za mzalishaji.

